

MBINU ZA KUFUNDISHA ISIMU YA KISWAHILI SEKONDARI
NA VYUONI

J.C. Kayuza

Lugha ni nini: Ni sauti bayana zilizokubaliwa na jamii kwa kuwasiliana. Ni sauti bayana kwani ni sauti moja moja zilizounganishwa ili kuleta maana katika jamii fulani.

k.m.	Kiswahili	-	Nyumba
	Kiingereza	-	House
	Kimalagasy	-	Ntrano

Sauti hizo bayana kwa jina lingine huitwa fonimu.

Fonimu ni kipande sauti chenye kuleta tofauti ya maana katika neno.

k.m. /p/aa /t/aa /s/aa

Alofoni ni matamshi mbalimbali ya fonimu. Kwa mfano tukiwa na fonimu /p/na ikiwa imo katika maneno pepo na mpira; katika pepo, /p/ ya, mwanzo inatamkwa kama (ph) yenye mpumuo. Katika neno la pili mpira /p/ inayotamkwa ni (p-) isiyo na mpumuo. Kwa hiyo kutokana na maneno hayo fonimu /p/ ina alofoni:

1	(ph)	3	(p)
2	(p-)		

KIINI NA SHINA

Kiini cha neno ni sehemu ndogo sana ya neno huwa haiwezi kugawanywa zaidi. Tuchukue kwa mfano neno "cheza." Kiini cha neno hili ni '-chez-' Neno hili haliwezi kuvunjwa-vunjwa zaidi ya '-chez-.' Kwa hiyo '-chez-' ni kiini.

Lakini ili tuweze kupata maana, zaidi sharti tuongeze mnyambuliko. Kwa hiyo mnyambuliko ni nyongeza ! a. '

Kwa hiyo neno 'chez - a' - cheza. Tunaweza kuongeza minya-

mbuliko mingine mingi. Kwa mfano:

chez	-	a	-----	cheza
chez	-	ea	-----	chezea
chez	-	esha	-----	chezesha
chez	-	eana	-----	chezeana

Hiyo yote hapo juu ni minyambuliko ya kiini '-chez-'

Katika lugha ya Kiswahili kiambisho ni mofimu isiyo huru ambayo huwa kabla ya kiini. Kwa mfano tukichukua kiini kile-kile - '-chez-', tukitaka kutumia neno hilo katika wakati uliopo nitasema NINACHEZA. Neno hili tungeweza kuligawa ifuatavyo:-

NI	-	NA	-	CHEZ	-	A
1		2		3		4

1/Ni/Kiambisho kinachowakilisha kiini. Kiambisho hiki huitwa cha Kiima. 2/Na/Kiambisho kinachowakilisha wakati. Kiambisho hiki kinaonyesha ni wakati gani kitendo kinatendeka. Kwa hiyo itawakilisha wakati uliopo. Kwa hiyo Kiambisho - NA - kinawakilisha wakati uliopo:

3/Chez/tumekwisha kizungumzia hiki ni kiini cha neno.
4/A/ya mwisho nayo tumekwisha izungumzia huo ni minyambuliko ambao huongezeka mwishoni kwa kiini.

Viambisho kwa kawaida huwa mwanzo wa kiini ni Minyambuliko hufuata baada ya kiini.

MSWAHILI

Neno mswahili kwa siku hizi lina maana nyingi. Maana zenyewe ni kama zifuatazo:-


- Mtu anayeishi pwani ya Afrika ya Mashariki mlaghai, mjanja
- Mwislamu
- huko Kenya neno hili lina maana ya Mtanzania
- mtu wa hali ya chini hapo tukiangalia tabaka za makazi kama zilivyoachwa na wakoloni. Nazo ni uzunguni, uhindini na uswahilini.
- Mwafrika tukiwa na maana ya cheo. Hii hasa hutokana

na zile sehemu ambazo labda Meneja alikuwa mtu wa taifa la kigeni. Tunaweza kusema Meneja tuliye naye ni mswahili tukiwa na maana ya mwafrika (au mtanzania mwenzetu)

- mzungumzaji wa Kiswahili fasaha.

ASILI YA NENO SWAHILI

Neno Swahili linatokana na neno "Sahel" neno hili ni la Kiarabu ambalo lina maana ya pwani ya Afrika ya Mashariki. Neno hili lilitumika na Waarabu walipofika pwani ya Afrika ya Mashariki waliwaita "Wasahel." Mashariki iliitwa "Kisahel." Kutokana na matamshi hayo ya nchi za kigeni baadaye neno hilo limekuwa Kiswahili.



Tunapozungumzia asili ya Kiswahili kuna haja ya kujiuliza kuwa hawa wenyeji waliokutwa na wageni walikuwa wakina nani. Tunapowazungumzia hawa wenyeji wa pwani hatuna budi vile vile kujikumbusha kuhusu kuingia kwa Wabantu Afrika ya Mashariki.

1. Kikundi cha kwanza cha Wabantu kilitoka Afrika ya Magharibi na kati na kufanya maskani yao kuzunguka Ziwa Victoria. Makabila ya Uganda na yale yanayozunguka ziwa Victoria kama Waganda, Wahaya n.k.

2. Kikundi cha pili cha Wabantu kilitoka Afrika ya Magharibi na kati na kilingia kati ya Ziwa Victoria na Tanganyika kupitia katikati ya Tanzania hadi pwani. Makabila ya Waha, Wanyamwezi, Wagogo, Wakaguru, Waluguru, Wazaramo na makabila ya mkoa wa Tanga yanatokana na kundi hili.

3. Kikundi cha tatu ni cha Wabantu kutoka Afrika ya Kusini na kupitia Zambia na Malawi hadi Kusini ya Tanzania. Makabila ya Zambia, Malawi kama Wabemba, Wanyasa na makabila ya Kusini ya Tanzania yanatokana na kundi hilo.

Kwa hiyo tunaamini kuwa wenyeji waliokutwa pwani na Waarabu walikuwa ni Wabantu. Na bila shaka lugha waliyokuwa wakizungumza ya Kiswahili kilikuwa ni Kibantu. Labda swali linalo-ambatana na usemi huo.

JE KISWAHILI NI KIBANTU AU KIARABU?

Tunapolinganisha lugha yeyote inatubidi tutumie misingi ifuatayo:-

1. MSAMIATI: Tujaribu kulinganisha maneno ya Kiswahili na yale ya lugha ya Kibantu:

KISWAHILI	mtu	maji	moto	chakula
1. <u>Cinyanja</u>	munthu	madzi	moto	chakudya
2. <u>Kizigua</u>	mntu	mazi	moto	nkhande
3. <u>Kizaramo</u>	muhu	maji	moto	ndigwa
4. <u>Kipogoro</u>	munthu	mashi	motu	chiboga
5. <u>Kinyakyusa</u>	umundu	amisi	umoto	ifindu
6. <u>Kisukuma</u>	munhu	minzi	moto	shiliwa

2. TUNGO: (Sentence pattern) Tujaribu vile vile kulinganisha sentensi ya Kiswahili na zile za lugha ya Kibantu.

KISWAHILI	Juma	anakula	ugali
1. <u>Cinyanja</u>	Juma	akudya	sima
2. <u>Kizigua</u>	Juma	adya	ugali
3. <u>Kizaramo</u>	Juma	koja	ugali
4. <u>Kipare</u>	Juma	ela	vughai
5. <u>Kipogoro</u>	Juma	kumkuliya	ubaga
6. <u>Kinyakyusa</u>	Juma	alilya	ugali
7. <u>Kisukuma</u>	Juma	aleliya	bugali

3. KITEMZI: Katika lugha ya Kiswahili.

Katika lugha ya Kiswahili Kitemzi huambatana na viambi-sho na mnyambuliko.

Kiswahili	1		2		3		4
	A	+	NA	+	CHEZ	+	A
Kizigua	A	+	Q	+	SEZIG	+	A

1. Kiambisho cha Kiima
2. Kiambisho cha wakati
3. Kiini
4. Mnyambuliko.

4. Mkubaliano (Agreement) kufuatana na Ngeli au upatanishi wa Kisarufi.

Kiswahili: (M) + toto (M) + dogo (M)

Kiswahili: (M) + toto (M) + dogo (M) + gonjwa
(Wa) (Wa) (Wa)

Kizigua (Mwa) + (M) + (M)

Kizigua (wa) + na (wa) + dodo (wa) + (nyonje)

Kutokana na sababu hizo mne za hapo juu, Kiswahili ni Kibantu na kama tunayo maneno ya Kiarabu hilo siyo jambo la kigeni, lugha yeyote haina budi ikope maneno kutoka lugha nyingine.

UKOFAJI WA MANENO

Lugha yeyote ile sharti ikope maneno kutoka lugha zingine. Na sababu za kukopa maneno hayo ni kama zifuatazo:-

1. **UTAWALA:** Kutokana na kutawaliwa kuna baadhi ya maneno ambayo yamekopwa na kuwa katika Kiswahili. Kutokana na utawala wa Waingereza tumepata maneno yafuatayo: Hospitali, Baiskeli, Dereva, reli, meli, Wajerumani maneno kama Akida, shule.
2. **BIASHARA:** Kutokana na biashara na nchi za kigeni kuna maneno ambayo tumeyakopa kutoka lugha ya Kihindi, ni kama laki, rupia, bagia. Maneno Kahawa, Msuri, Kiarabu ni tendeleo, Maneno ya Kingereza ya biashara ni shati, radio, friji, sinema.
3. **UTAALAM:** Kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia kuna baadhi ya maneno ambayo tunayatumia katika Kiswahili. Maneno kama Fonimu, Alofoni, Mofimu yana asili ya lugha za kigeni kwa vile yanatumika katika Kiswahili kwa hiyo matamshi yako katika Kiswahili.
4. **DINI:** Kutokana na dini za kigeni tumeweza kukopa maneno ambayo tunayatumia katika Kiswahili. Maneno kama alfajiri, alasiri, Korani Biblia yametokana na sababu hizo.
5. **KASUMBA:** Maneno yanayoingia katika Kiswahili kutokana na kuathiriwa k.m. dish, disko, msosi, muvi,, fresh, sista, anko.

MIUNDO MBALIMBALI KATIKA SENTENSI ZA KISWAHILI

1.	Juma		anaimba	wimbo
	Jina		kitenzi	jina
2.	Juma	anaimba		
	Jina	kitenzi		
3.	Asha	mzuri		
	Jina	kivumishi		
4.				
	Juma	anakwenda	Mjini	polepole
	Jina	kitenzi	kielezi	kielezi

UAINISHAJI WA SENTENSI ZA KISWAHILI

Sentensi ni fungu la maneno lenye maana kamili. Kwa mfano sentensi # Ali Juma anaimba wimbo. Sentensi hiyo inaweza kuainishwa katika njia zifuatazo:-

1. Juma anaimba wimbo

Kifungu Nomino	Kifungu Tendo
-------------------	---------------

2. Juma Anaimba wimbo

Kiima	Kiarifu
-------	---------

3. Juma anaimba wimbo

Jina	Kitenzi	Jina
------	---------	------

4. Juma anaimba wimbo

S → Kifungu Nomino + Kifungu Tendo


S → Jina + Kitenzi + Jina

S → Jina + Kiambisho
cha
Kiima + Kitenzi + Jina

S → Jina + Kiambisho
cha
Kiima + Kiambisho
cha
wakati + Shina + shina + Jina

S → Jina + Kiambisho
cha
Kiima + Kiambisho
cha
wakati + Kiini Mnyambuliko
Jina

S → Juma a + na + imb + a wimbo



LAHAJA

Lahaja (dialect) lazima kuwa na jumuiya ya lugha km Kiswahili, Kifaransa, Kiingereza. Lakini kutokana na sehemu ambazo watu wanaishi na umbali iliopo kati yao basi matamshi ya lugha hiyo moja yanatofautiana.

- k.m. (1) Kingereza cha Kiskochi
 (2) Kingereza cha Kiamerika
 (3) Kingereza cha Kitanzania

au Cigogo - kwa ajili ya umbali walionao kuna wengine wanaitwa Wanyambwa, Wahehe, Wakaguru. Lugha zote hizo ni moja ingawaje matamshi yanatofautiana. Kwenye lugha ya Kiswahili kuna lahaja zifuatazo: Kiunguja, Kimtang'ata, Kipemba, Kimvita, Kingare, Kijomvu n.k.

USANIFISHAJI WA LUGHA

Tunapotaka kusanifisha lugha: sharti tuwe na lahaja (vilugha) kwa mfano katika Kiswahili lahaja zilizoshughulikiwa wakati

huo na Interterritorial Language Committee zilikuwa ni Chichifundi, Kivumba, Kiunguja, Kimtang'ata, Kipate, Kingare.

Lahaja inayochaguliwa na kusanifishwa sharti kwamba iwe inazungumzwa na wengi. Wakati huo Kiunguja kilikuwa kinazungumzwa na wengi.

Pili lahaja inayochaguliwa sharti iwe katika sehemu ambayo kuna makutaniko. Mahali ambapo watu huja mara kwa mara.

Tatu ni kuwa lahaja inayochaguliwa sharti iandikwe.

Nne lahaja hiyo sharti ifuate sheria. Sheria ni kama Jina, Kitenzi na Kivumishi katika sentensi kamili.

Tano lahaja hiyo sharti ijitosheleze. Lahaja iweze kuwa na msamiati wa kutosha bila ya kutegemea lugha nyingine.

3. REJESTA - Matumizi ya lugha kutegemeana na watu. Kwa mfano lugha ya maproffessa - Rejesta yao. Na vibarua makuli wana rejesta na maneno watakayoyazungumza yanawafaa wao zaidi. Kwa mfano wakiwa wataalam wa Isimu wanazungumza maneno kama mofimu, fonimu yata-sikiKa. Hii ni lugha ambayo wao wanaelewana. Vile-vile makuli baharini nao watakuwa na lugha yao lugha ya wataalam wa Isimu na hao makuli tunaziita REJESTA.

UMBO LA NDANI NA LA NJE

Nadharia ya umbo la ndani na la nje imezungumziwa kwa kirefu na Noam Chomsky ambaye tunaweza kumwita bingwa wa nadharia hiyo. Wataalam wengine ni Owen Thomas, J.P.B. Allen na Van Buren, na Frederick A. Jacobs na Peter Rosenbaum. Hawa ndio wakongwe kwenye nadharia hiyo. Mimi nitatumia nadharia zao katika lugha yetu ya Kiswahili.

Kwanza tukiziangalia sentensi zote tunazozitamka mara nyingi huwa zina maana na hutoa ujumbe wa aina fulani. Wataalam hao niliowataja hapo juu wanasema kuwa sentensi yoyote tunayozitamka yenye maana iko katika umbo la ndani la sentensi. Umbo hili la ndani mara nyingi huwa halina maana. Naomba sasa tuangalie mfano wa sentensi ifuatayo:-

1. Amelala

Sentensi hiyo ina maana kuwa mtu amelala. Sentensi hiyo tunasema kuwa iko kwenye "Umbo la Nje" kwani ina maana.

Je unaweza kuitafuta na kuipata asili ya sentensi hiyo ambayo tunaweza kuiita umbo la ndani?

2. -lal-

Sasa kama -lal- ni kiini kimwezaji kufikia "Amelala," kwa hiyo kiini kimepitia hatua mbalimbali kisarufi. Tujaribu kuziangalia hatua hizo moja moja.

3. -lal^{*} a - lala
Kiini Mnyambuliko - shina

lakini sentensi yetu inazidi kutueleza kuwa "Amelala" na siyo "lala" kwa hiyo bila shaka hatua inayofuata ni ya kuongeza kiima.

4. Mtu lala
Kiima shina

Inabidi tuongeze kiambisho cha Kiima ambacho kinaonyesha kuwa mtu anatenda kitendo. Kwa hiyo baada ya kuongeza Kiambisho, cha kiima sentensi yetu itakuwa:

5. Mtu a + lala
Kiima Kiambisho + Shina
 cha
 Kiima

Sentensi hiyo bado haijakamilika kwani tuna Kiima, Kiambisho cha Kiima cha Shina. Bado haijawa sentensi kwani bado haiteti maana na vile vile haionyeshi wakati gani kitendo hicho kinatendeka.

Kuna umuhimu wa kuongeza Kiambisho cha wakati. Kiambisho cha wakati kwa kawaida hufuatia Kiima. Sentensi yetu kama tulivyoiona hapo awali inaonyesha wakati uliopo. Kwa hiyo itabidi tuongeze Kiambisho cha wakati /me/ ili iwe:-

6. Mtu - a + me + lala
Kiima Kiambisho Kiambisho Shina
 cha kiima cha wakati

Sentensi yetu imekamilika kwani karibuni nyongeza zote zimo na ndizo zinazotufanya tupate maana kuwa:-

7. Mtu amelala
Kiima kitenzi

Hata hivyo kwenye sentensi yetu tunayoitumia kwenye majadiliano haya haikuwa na neno "mtu" ambalo ni Kiima. Kwa

hiyo ni dhahiri kuwa neno "mtu" limeondolewa na ndiyo maana tukabakiwa na "Amelala".

Kwa hiyo itabidi sentensi ya 8 "mtu amelala" ipitie hatua ya mwisho. Na hatua hiyo ni kuondoa neno "mtu". Kwa hiyo sentensi yetu itakuwa "amelala" (Tunaondoa Kiima "Mtu".)

1. - lal - (ongeza mnyambuliko wa + a)
 Kiini Shina
2. lala (weka Kiima mwanzoni cha mtu)
3. Mtu ... lala (Ongeza Kiambisho cha Kiima)
4. Mtu a ... lala (Ongeza Kiambisho cha wakati uliopo)/me/.
5. Mtu a + me lala + (Dondosha neno "mtu").
6. Amelala

MAUMBO

Tunapojadili maumbo tunaanzia ngazi ya juu na kuteremka hadi ngazi ya chini.

1. Sentensi ndiyo ngazi ya juu kabisa ya maumbo k.m. sentensi ifuatayo:-

 Juma analima shamba la baba yake

2. Kirai ni ngazi ya pili ya maumbo kwa mfano sentensi:-

 Juma analima shamba la baba yake

Sentensi hii ina virai viwili navyo ni:

1. Juma
2. Analima shamba la baba yake.

Kila Kirai kina maana kamili k.m. Juma inawezekana anaitwa. Analima shamba la baba yake kinaeleza kitendo kinachotendeka

3. Kishazi ni ngazi ya tatu. Kishazi fungu la maneno linakuwa halina maana likiwa peke yake. k.m. katika sentensi:-

 Juma analima shamba la baba yake

la baba yake ikiwa peke yake haina maana hata kidogo.

4. Ngazi ya nne ni NENO katika sentensi:-

Juma analima shamba la dada yake

Sentensi hiyo ina maneno sita:-

Juma	Analima	shamba
1	2	3
la	baba	yake
4	5	6

5. Mofimu ndiyo ngazi ya mwisho ya maumbo. Neno Mofimu ni tamko dogo lenye maana Kisarufi kwa mfano kwenye sentensi:-

Juma	a	na	lim	a	shamba	la
1	2	3	4	5	6	7
baba	ya	ke				
8	9	10				

Sentensi hiyo ina mofimu kumi. Pia katika kuondoa utata kati ya neni mofimu na fonimu. Tunaweza kulinganisha sentensi hiyo ina mofimu ngapi na ina fonimu ngapi.

Mofimu;	Juma	a	na	lim	a	shamba
	1	2	3	4	5	6
	la	baba		ya	ke	
	7	8		9	10	

Fonimu ni kipande sauti chenye kuleta tofauti ya maana kwa hiyo sentensi.

J U M A	a	n	a	i	m	a		s	h	a		m	b	a		l	a
1	2	3	4	5	6	7	8	9	10	11	12	13	14	15	16	17	18
	b	a		b	a						y	a		k	e		
	19	20	21	22							23	24	25	26			

Kwa hiyo sentensi hiyo ina fonimu 26. Pia tunaweza kujiuliza tofauti iliyopo kati ya; Mofimu na silabi ni ipi. Tukiangalia sentensi ile ile:-

MOFIMU:	Juma	a	na	lim	a	shamba	la
	1	2	3	4	5	6	7
		baba	ya	ke			
		8	9	10			

Kwa hiyo sentensi ina mofimu 10.

Tukiangalia SILABI kwenye sentensi hiyo:-

Juma	a	na	li	ma	sha	mba	la
1 2	3	4	5	6	7	8	9
	ba	ba	ya	ke			
	10	11	12	13			

Kwa hiyo sentensi ina silabi 13. Wakati sentensi ina MOFIMU 10 sentensi hiyo hiyo ina SILABI 13.

MOFIMU KATIKA KISWAHILI

Tunapojadili kuhusu mofimu mfano ambao unafaa ni ule wa kiteenzi katika Lugha ya Kiswahili.

k.m. A N A L I M A

Neno hilo tunaweza kuligawa katika mofimu zifuatazo:-

(A)	(NA)	+	(LIM)	+	(A)
1	2		3		4

Kama zinavyoonyeshwa hapo juu ni mofimu nne:-

1. A - ni mofimu yenye kuwakilisha kiima.
2. NA - ni mofimu inayowakilisha wakati.
3. LIM - ni mofimu inayowakilisha kiini.
4. A - ni mofimu inayowakilisha Mnyambuliko.

AINA ZA MOFIMU

1. Mofimu huru - ni mofimu ambayo huweza kuwa peke yake bila ya viambisho k.m. majina kama Juma, Ali, Mbuzi, Tembo.
2. Mofimu tegemezi - ni mofimu ambazo haziwezi kusimama pekee kwa mfano viambisho katika Kiswahili.

(A)	(NA)	(LIM)	(A)
1	2	3	1

Mofimu zote nne ni tegemezi, mofimu hizo zote haziwezi kusimama peke yake.

3. MOFIMU CHANGAMANO:- Ni mofimu tegemezi zikiwa zimechangamanishwa kwa mfano kwenye kitenzi cha Kiswahili kunakuwa na:-

(A)	(NA)	(LIM)	(A)
Kiima	Kiambisho cha wakati	Kiini	Mnyambulik

Viambisho pamoja na kiini vimechangamanishwa ili kuwa na kitenzi ambacho ni Mofimu changamano.

4. Mofimu Mwambatano ni mwambatano wa mofimu mbili huru. Kwa mfano:-

Mwana	+	Chuo
Jina		Jina
Mwenda	+	Kwao
Jina		Kivumishi

5. Mofimu kapa - mofimu kapa

Inapatikana kwenye wingi wa baadhi ya majina. Kwa kawaida katika Kiswahili kuna mofimu za Umoja na Wingi. k.m. Mtu - Watu (M) kwenye umoja na (Wa) kwenye wingi. Lakini kuna baadhi ya majina kwenye Umoja na Wingi hakuna mofimu inayoongezwa. k.m. neno /mbuzi/ kwenye umoja ni /mbuzi/ na kwenye wingi ni /mbuzi/. Kwa mfano tunaweza kusema Mbuzi yumo zizini (umoja) na kwenye wingi tukasema Mbuzi wamo zizini. Kwa hiyo umoja na wingi ni mbuzi. Tunaweza kusema:-

Umoja

Mbuzi

Wingi

Mbuzi

Vile vile tunaweza kusema kwa mfano Mbuzi huyu
Mbuzi hawa

KIFUNGU NOMINO

Wataalam wengi wamejaribu kujadili kwa kirefu maana ya Kifungu Nomino kati ya lugha mbalimbali. Nami katika kuchokoza majadiliano hayo nimeona nami niitumie lugha ya Kiswahili kwa mjadala huo.

Kwanza: nitafsiri na kutoa maana ya kifungu Nomino. Kifungu Nomino ni sehemu ya jina au mtenda. Nitachukua mifano ifuatayo ya sentensi ili kuchambua kifungu Nomino.

1. Juma analima shamba
2. Juma mvivu amepigwa sana
3. Analima
4. Kaka Juma anapiga pasi
5. Juma aliyeugua sana amefariki

Katika hizo sentensi tano hapo juu, tunaweza kuzigawa ifuatavyo:-

- | | | | |
|----|---------------------|---|----------------|
| 1. | Juma | / | analima shamba |
| | Kifungu Nomino | / | kifungu tendo |
| 2. | Juma mvivu | / | amepigwa sana |
| | Kifungu Nomino | / | Kifungu tendo |
| 3. | Ø | / | analima |
| | Kifungu Nomino | / | Kifungu tendo |
| 4. | Kaka Juma | / | anapiga pasi |
| | Kifungu Nomino | / | Kifungu tendo |
| 5. | Juma aliyeugua sana | / | amefariki |
| | Kifungu Nomino | / | Kifungu tendo |

Kwa hiyo vifungu Nomino katika sentensi hizo tano hapo juu ni:-

1. Juma
2. Juma mvivu
3. \emptyset
4. Kaka Juma
5. Juma aliyeugua sana

Tunaweza kusema:-

1. Juma /
Jina /
2. Juma mvivu /
Jina Kivumishi
3. \emptyset
4. Kaka Juma /
Kivumishi Jina
5. Juma aliyeugua sana
Jina Kitenzi Kielezi
Saidizi

Kwa hiyo tunaweza kusema katika sentensi tano hapo juu tunaweza kupata muundo ufuatao:-

1. Jina
2. Jina + Kivumishi
3. \emptyset
4. Kivumishi + Jina
5. Jina Kitenzi Kivumishi
Saidizi

Kwa kifupi tunaweza kupata muundo ufuatao:-

(Kivumishi) (Jina) (Kivumishi) (Kitenzi) (Kielezi)
() () () (Saidizi) ()
(\emptyset) (\emptyset) (\emptyset) (\emptyset) (\emptyset)

Kutokana na sentensi za hapo juu kifungu Nomino katika Kiswahili huwa:-

(Kivumishi)	(Jina)	(Kivumishi)	(Kitenzi)	(Kielezi
()	()	()	(Saidizi)	()
()	()	()	()	()
(Ø)	(Ø)	(Ø)	(Ø)	(Ø)
V	N	V	T _S	E

KIFUNGU TENDO KATIKA KISWAHILI

Baada ya mjadala wa kifungu Nomino katika Kiswahili kuna haja ya kujadili kifungu Tendo. Na nitatumia sentensi zile zile nilizotumia katika Kifungu Nomino.

1. Juma analima shamba
2. Juma mvivu amepigwa
3. Ø Analima
4. Kaka Juma anapiga pasi
5. Juma aliyeugua sana amefariki

Kwanza sentensi za hapo tuzigawe katika kifungu Nomino na Kifungu Tendo.

1.	Juma	ANALIMA SHAMBA
	Kifungu Nomino	KIFUNGU TENDO
2.	Juma mvivu	AMEPIGWA
	KIFUNGU NOMINO	KIFUNGU TENDO
	Ø	ANALIMA
4.	Ø	KIFUNGU TENDO
	Kaka Juma	ANAPIGA NGOMA
5.	Kifungu Nomino	KIFUNGU TENDO
	JUMA aliyeugua	AMEFARIKI

Katika sentensi za hapo juu tuchambue vifungu tendo vya sentensi zote.

1.	Analima	SHAMBA
	Kitenzi	Jina
2.	Amepigwa	
	Kitenzi	
3.	Analima	
	Kitenzi	
4.	Anapiga	Ngoma
	Kitenzi	Jina
5.	Amefariki	
	Kitenzi	

Kwa hiyo tunaweza kusema kuwa katika sentensi hizo tano vifungu vya tendo ni kama ifuatavyo:-

- | | | |
|----|-----------|------|
| 1. | (Kitenzi) | Jina |
| 2. | (Kitenzi) | |
| 3. | (Kitenzi) | |
| 4. | (Kitenzi) | Jina |
| 5. | (Kitenzi) | |

Kwa kifupi, kutokana na sentensi hizo tunaweza kusema kuwa kifungu 'tendo katika sentensi hizo ni:-

(Kitenzi)	(Ø)
	()
	(Jina)
T	N

MUUNDO UNAOWEZEKANA KATIKA SENTENSI ZA KISWAHILI:

Iwapo tuna sentensi nyingi za lugha moja tunaweza kweli kutoa muundo mmoja kwa sentensi hizo zote?

Tujaribu, kuziangalia sentensi zifuatazo:-

1. Juma mgonjwa amelala
2. Anamtoa wimbo

3. Sukari ni mbaya sana
4. Ugonjwa wake umezidi
5. Masomo yamezidi ugumu

Sasa tuangalie miundo ya sentensi hizo zote:-

1. Jina Kivumishi Kitenzi
2. Kitenzi Jina
3. Jina Kitenzi Kivumishi Kielezi
4. Jina Kimilikisho Kitenzi
5. Jina Kitenzi Jina

Kutokana na miundo hiyo sentensi hizo tano tunaweza kupata miundo ifuatayo:-

1. Jina Kivumishi Kitenzi
2. Kitenzi Jina
3. Jina Kimilikisho Kivumishi Kitenzi Kivumishi Kielezi

Kutokana na miundo hiyo sentensi hizo tano tunaweza kupata miundo ifuatayo:-

(Jina)	(Kimilikisho)	(Kivumishi)	(Kitenzi)	(Kivumishi)	(Kielezi)
(Ø)	(Ø)	(Ø)	(Ø)	(Ø)	(Ø)
N	T(Kumiliki)	V	T	V	E

Tuone tunaweza kupata muundo gani unaokubaliana na muundo wa hapo juu:-

"Ugonjwa wake mbaya umezidi sana."

KITENZI KATIKA LUGHA YA KISWAHILI

Katika lugha ya Kiswahili, Kitenzi huwakilishwa mara zote kama shina kwa mfano / cheza / ni shina ambalo cheza (Kiini mnyambuliko. Hali hii imo katika vitenzi vyote vya Kiswahili na lugha za Kibantu.

Pili ni kuwa Kitenzi kinapotumiwa kwenye sentensi hakina budi kiwe na viambisho. Kwa mfano nataka kutumia Kitenzi /cheza/ katika wakati uliopo sentensi itakuwa ifuatavyo:-

Mimi ninacheza

Katika kuichambua zaidi sentensi hiyo itakuwa ifuatavyo:-

Mimi	ni	na	/chez/	a
Kiima	Kiambisho	Kiambisho	Kiini	Mnyambuliko
	cha	cha		
	Kiima	wakati		

Viambisho na mnyambuliko ni mofimu tegemezi wala siyo huru. Tatu ni kuwa Kitenzi katika Kiswahili kinaweza kuwa sentensi kamili. Kwa mfano:-

Sentensi ile ile hapo juu: /Mimi ninacheza/

Katika Kiswahili kiima cha /Mimi/ kinaweza kikaondolewa na sentensi ikiwa na maana ile ile. Kwa mfano:-

/Mimi ninacheza/ Ondoa Mimi inabaki

/Ninacheza/

Nne Kitenzi katika Kiswahili huweza kunyambulika zaidi. Tuchukue mfano wa tendo letu lile lile la /cheza/, tunaweza kupata minyambuliko ifuatayo:-

1. Chez a ----- cheza
2. Chez ea ----- chezea
3. Chez eana ----- chezeana
4. Chez ewa ----- chezewa
5. Chez eka ----- chezeka

Kwa hiyo hāyo ni mambo muhimu tunaposhughulikia Kitenzi katika lugha ya Kiswahili na lugha za Kibantu.

MAMBO MUHIMU KATIKA KAMUSI

Kamusi kikiwa ndicho chombo muhimu katika lugha, haina budi iwe na mambo muhimu yafuatayo:-

1. Herufi sahihi za neno

- Kwa yeyote anayejifunza Lugha ya Kiswahili atapenda kuona herufi sahihi za neno. Kwa hiyo kama alikosea kuliandika, mahali pekee ambapo anaweza kupata herufi sahihi za neno hilo ni kwenye Kamusi tu.

2. Matamshi sahihi

- Kwa yule anayejifunza Lugha hana budi apate matamshi sahihi kutokana na kunukuu, kwa bahati nzuri, Kiswahili kinatamkwa kama kinavyoandikwa kwa hiyo itakuwa ni rahisi kwa anayejifunza Lugha kupata matamshi sahihi kutokana na alama za kifonetiki.

3. Kuonyesha aina ya neno kama ni tendo au jina au Kivumishi na kielezi

- Kamusi ionyeshe kama neno ni jina au tendo k.m. nyumba(Nomino) akili(Nomino ya maarifa). Hii ni muhimu sana katika kamusi kwa sababu itaonyesha wazi kuwa neno ni Nomino au Kivumishi au Kielezi. Kwa mfano mtoto mvivu Mtoto(Jina) na mvivu(Kivumishi).

4. Minyambuliko

- Kamusi ionyeshe jinsi neno linavyoweza kunyambulika. Kwa mfano itakuwa vizuri kama neno /cheza/ litaonyeshwa pamoja na neno /mchezo/ ili anapojifunza aweze kuona uhusiano uliopo kati ya /cheza/ na /mchezo/. Minyambuliko mingine kama /chezea/ /kitabu/ /mkutubi/.

5. Maana

- Kamusi ionyeshe maana ya neno kwa sababu anayejifunza Lugha atapenda kuelewa maana ya neno. Na hasa kufuatana na utamaduni. Kwa mfano kunya ni kitendo cha kwenda choo, lakini ni mara chache tukikaa na watu kama Wakwe tunaweza kusema "samahani Mkwe mimi ninakwenda kunya" Bila shaka tutasema kuwa "samahani Mkwe mimi ninakwenda uani." Hii yote ni kuipa hadhi lugha kufuatana na utamaduni wetu wa Kiswahili.

6. Mgawanyo wa silabi

- Kwa anayejifunza Kiswahili atapenda kuona jinsi silabi za neno zinavyogawanyika. Kama tunavyoona Kiswahili hakuna shida sana. Mara nyingi silabi ni konsonanti na irabu. Na iwapo irabu mbili zinafuatana basi kila irabu itakuwa ni silabi mbili: Ki ti /kiti/ ni silabi.

1 2

Na katika neno mu / u / ndo / hapo pana silabi

1 2 3

mu / u / ndo

1 2 3

Hii ni muhimu sana kwa mtu anayejifunza Kiswahili kwa sababu Lugha zingine zina nadharia tofauti za silabi.

7. Maneno yanayokwenda pamoja na hilo neno

- Ni muhimu kuonyesha kwenye Kamusi baadhi ya maneno yanayokwenda pamoja k.m. mpira lina-kwenda pamoja na mpira wa miguu, mpira wa vinyoya, mpira wa vikapu, mpira wa wavu, mpira wa vigongo n.k.

Na hii itamsaidia anayejifunza Lugha kuelewa

8. Maana ya neno kufuatana na utamaduni

- Inatubidi tuonyeshe maana ya neno wazi wazi. Mfano neno "mto" linaweza kutegemeana na maana mtu alipo. Kwa mfano mtoto aliyekulia Mkoa wa Dodoma, ukimweleza mto yeye atafikiria ile mito ya misimu ya Dodoma ambayo ni makorongo. Lakini kijana wa Rufiji, ukimtajia mto, yeye atapata hisi zote za mto Rufiji. Kwa mfano unapofurika samaki na mpunga unaolimwa kwenye bonde hilo.

9. Maana mbalimbali za neno hilo hilo moja

Kwa mfano tukichukua neno /kaa/ - kaa - kaa la moto

- kaa - kaa kitini

- kaa - mnyama wa baharini.

Kuna umuhimu kwa Kamusi kuzielezea maana hizo zote mbalimbali za neno kaa. Tunachotaka ni kuwa yule anayejifunza Lugha ya Kiswahili alitumie neno li postahili, siyo atumie ovyo na kuyachafua matumizi bora ya Kiswahili.

10. Matumizi ya methali na nahau za Kiswahili

Kamusi ionyeshe methali na nahau kwa jinsi zinavyotumika kwa sababu hiyo ndiyo njia pekee ambayo huonyesha kuwa Lugha ni tajiri, kwa mfano:- Unaagana na mtu, ukamwambia "Milima haikutani" msemaji akiwa na maana kuwa ingawa wameagana lakini siku moja bila shaka watakutana mahali. Lakini ingekuwa milima ndiyo kama ingekuwa na uwezo wa kusema ingesema kuwa haikutani. Au kusema nahau ifuatayo:-


Nimekutana na Jamaa ambaye ameibugia chumvi nyingi. Ikiwa na maana kuwa mtu aliyeishi kwa muda mrefu sana au mtu aliyeishi kwa miaka mingi.

11. Vipimo:

Ni aina gani ya vipimo inayotumika kwa mfano kama tunatumia vipimo vya mita kuna haja ya kuvionyesha na kutumia vipimo vya inchi, inabidi kuvionyesha na hata vipimo vya nguo; kwa mfano tukisema shati kubwa na dogo. Tunajaribu kuonyesha ni inchi ngapi au mita ngapi ili anayenunua nguo hizo afahamu kuwa shati la kati lina ukubwa gani.

12. Matumizi ya picha kuelezea neno ni muhimu sana

Lakini picha haina budi ionyeshe kikamilifu kwa mfano:-



Kwa mfano picha hiyo hapo juu inaweza ikapotosha kama itakuwa na maana ya meli. Maana yule anayejifunza anaweza akaona meli yenyewe na asiitambue kuwa ni meli. Lakini anaweza kuona kaburi lenye msalaba akafikiri meli. Kwa hivoni muhimu kwa picha kuonyesha wazi wazi mambo hayo. Pia rangi inayopakwa kwenye picha lazima ifanane na hali halisi ya kitu kinachozungumziwa. Kwa mfano hatuwezi kuchora picha ya ng'ombe wa rangi ya njano kwa sababu hayupo.

13. Herufi nene

Herufi ziwe kubwa zinazosomeka. Herufi zisiwe ndogo ndogo sana na kuumiza macho. Herufi ziwe nene zenye wino mzito wa kusomeka.

14. Historia ya neno

Kuna umuhimu pia kuonyesha kuwa neno hilo linatokana na Lugha nyingine kwa sababu inasaidia kupata maana kamili. Kwa mfano neno "meli" linatokana na wageni neno mail la Kiingereza ambalo wageni walipokuja hapa walilitumia kwa barua ambazo usafiri wa wakati huo ulikuwa wa meli. Kwa hiyo meli ikija ilileta (mail) barua; kwa hiyo katika kurahisisha matamshi yakawekwa matamshi ya Kiswahili ya "meli"

15. Mgawanyo wa SILABI - Kamusi ionyeshe jinsi silabi zina-
vyogawanywa. Kwa mfano katika Kiswahili neno baba lina
silabi mbili. ba/ba.

NADHARIA YA TAFSIRI

Tunapotaka kutafsiri lugha moja hadi lugha nyingine, yule anayetafsiri hana budi azifahamu lugha zote mbili kinaganaga. Kwa mfano iwapo mtu anataka kutafsiri Kiingereza hadi Kiswahili hana budi azifahamu lugha zote barabara.

Kuzifahamu barabara, kwanza ni kuwa na msamiati wa kutosha. Msamiati huo uweze kutosheleza barabara kila neno ambalo unali tafsiri. Kwa mfano tuangalie sentensi hiyo ifuatayo:-

The cake was palatable

Sentensi hiyo kwa mtu mwenye msamiati hafifu atasema tu;

Keki ilikuwa nzuri

Swali la kujiuliza ni kama neno "palatable" lina maana sawa na nzuri, kama ilivyotafsiriwa.

Itabidi tupate neno ambalo lina maana

Itabidi tupate neno ambalo lina maana ya "palatable" kufuatana na hali ya keki. Bila shaka neno hili lina maana ya utamu wa keki, wakati inapopita kinywani. Kwa hiyo neno linalostahili hapo ni "tamu." Kwa hiyo ile sentensi ya Kiingereza

The cake was palatable

tafsiri yake itakuwa

Keki ilikuwa tamu.

Hatua ya pili ya kuijali sana wakati tunapotafsiri ni kuzielewa sheria za lugha zote mbili barabara. Kila lugha ina miiko yake. Sentensi haina budi ifuate mpangilio fulani, bila ya kufuata mpangilio huo haitakuwa na maana.

Kwa mfano sentensi:-

Tobacco	Authority	of	Tanzania
1	2	3	4

Hapo ikitafsiriwa kufuata muundo wa Kiingereza, tuta-pata sentensi ifuatayo:-

Tumbaku	Mamlaka	ya	Tanzania
1	2	3	4

Sentensi hiyo hapo juu haikubaliki kwa sababu mpangilio huo hapo juu haukubaliki katika sentensi za Kiswahili. Hii inaonyesha wazi mpangilio wa sentensi za Kiingereza ambavyo hutofautiana na ule wa sentensi za Kiswahili.

Kwa hiyo sentensi yetu ya Kiingereza:-

The Tobacco	Authority	of	Tanzania
1	2	3	4

Tafsiri yake siyo;

Tumbaku	Mamlaka	ya	Tanzania
1	2	3	4

tafsiri sahihi ni:-

Mamlaka	ya	Tumbaku	Tanzania
2	3	1	4

Jambo la tatu la kuangalia ni matumizi ya lugha kufuatana na mahali. Kwa mfano tukiwa kiwanjani tukiangalia mpira na tukafurahishwa na udakaji mpira wa Juma, tunaweza kusema:-

Juma ni nyani

Hapo neno "nyani" halina maana kuwa Juma ni nyani, mnyama bali ule ubingwa wake wa kunyaka mpira kiwanjani ndio unaomfanya aitwe nyani. Kwa hiyo kwenye tafsiri hatutasema Juma is a baboon.

Kwa sababu sentensi ya "Juma ni nyani" haina maana hiyo. Kwa hiyo itabidi tupate maana ya sentensi kufuatana na mahali. Kwa sentensi hiyo ikitafsiriwa ikiwa na maana ya ubingwa wa Juma katika kunyaka mpira itakuwa:-

Juma is a skillful goalkeeper

Sentensi hiyo hapo juu inatuthibitishia kwamba ubingwa wa kudaka alio nao huyu kipa Juma ndio hasa hapa tumepata maana ya hapo juu.

Kwa hiyo tufanyapo tafsiri za aina yoyote ile inabidi tuzingatie mambo yafuatayo:-

1. Msamiati
2. Sheria za lugha
3. Maana ya sentensi au habari kabla ya kuitafsiri.

Bila ya kuzingatia mambo hayo matatu hapo juu, tutaendelea kutoa tafsiri zisizokuwa na maana hata kidogo.

MAKTABA
TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI